# RASIMU YA KATIBA NA MWELEKEO WA UHURU NA UFANISI WA SERIKALI ZA MITAA




**Mtazamo wa Policy Forum**

**Baada ya Uchambuzi wa Rasimu**

Rasimu ya Katiba mpya na Mwelekeo wa Uhuru na Ufanisi wa Serikali za Mitaa


**Kimeandaliwa na**

| | |
|---|---|
| Israel Ilunde | YPC (youth Partnership Worldwide) |
| Asna Msana | KEPA |
| Regina Katabi | MUDUGU - WACOD |
| Alex Ruchyahinduru | Policy Forum Secretariat |
| Hebron Mwakagenda | The Leadership Forum |

**Kimehaririwa na kupitiwa na**

Humphrey Polepole - Mjumbe wa Tume ya Katiba

**Mchora Katuni:**

Nathan Mpangala



Kimechapishwa na Policy Forum

Toleo la kwanza - Aprili 2014

ISBN: 978-9987-708-13-0



©Policy Forum



Kimesanifiwa na kupigwa chapa na

Jamana Printers Limited
P.O. Box 5584
Dar es Salaam, Tanzania

# Dibaji

Kitabu hiki ni mfululizo wa mchango wa Policy Forum kwenye mchakato wa kuandika katiba mpya hapa nchini Tanzania toka uanze mnamo Disemba 2010, kitabu hiki ni cha tatu katika mfululizo huo wa vitabu vilivyotolewa na Policy Forum kuchangia uelewa.

Kitabu cha kwanza na maarufu sana kilikuwa *Mwongozo wa Katiba kwa Raia* ambacho kilitolewa mapema wakati mchakato unaanza tu, kitabu cha pili kilikuwa *Katiba Mpya na Ufanisi wa Serikali za Mitaa* ambacho kilitolewa mara baada ya rasimu ya kwanza kutolewa na Tume na kitabu hiki ambacho ni cha tatu kinasisitiza tena juu ya suala la serikali za mitaa katika katiba na kimetolewa mara baada ya rasimu ya pili kutolewa. Policy Forum inatambua kuwa serikali za mitaa sio suala la Muungano na kwamba suala hili litashughulikiwa na serikali washirika mara baada ya kukamilisha mchakato wa kuandika katiba ya Jamhuri ya Muungano lakini kwa kutambua kuwa bila kupigia kelele masuala kadhaa muhimu yanaweza kusahaulika hivyo tumeona tuonyeshe nini kipo kwenye rasimu ya pili ya katiba kuhusiana na serikali za mitaa ili kuwafahamisha wabunge wa bunge la katiba na wananchi kwa ujumla wajue msimamo uliopo kwenye rasimu ya katiba.

Ni matarajio yetu kuwa kitabu hiki kama vilivyo vitabu vyetu vingine kimetumia lugha rahisi na picha ambavyo vinaweza kueleweka kwa urahisi na mwananchi mtanzania wa kawaida hivyo basi kitachangia sana uelewa kwenye mchakato unaoendelea na hasa katika hatua hii ya bunge maalum la katiba na kuelekea upigaji kura ya maoni au maamuzi hapo baadaye.

Tunawaomba wasomaji wetu wapate muda wa kusoma na kutafakari ili muda ukifika wa kushughulikia masuala ya serikali za mitaa Tanganyika au Zanzibar basi wote tuwe pamoja na kuweka mambo kama vile tunavyotaka yawe.

**Semkae Kilonzo**
**Mratibu**

# 1. UTANGULIZI

## 1.1 Maana ya Katiba:

Kumekuwepo na maana tofauti tofauti juu ya maana ya katiba. Kwa mujibu wa sheria namba 8 ya Mabadiliko ya katiba sura ya 83(2012); neno katiba likianza na herufi 'k' ndogo lina maana tofauti na pale katiba neno hili linapoanza na herufi 'K' kubwa. Sheria hii inatoa fasiri ya *"katiba" kwa kusema maana yake ni sheria ya msingi, iliyoandikwa au isiyoandikwa, ambayo inaweka mfumo wa taifa kwa kuainisha misingi ya taifa ambayo jamii italazimika kuifuata, mgawanyo wa madaraka na majukumu ya mihimili mikuu ya dola, kwa kuainisha muundo wa serikali, bunge na mahakama, usimamizi wake mgawanyo na ukomo wa mamlaka ya vyombo mbalimbali vya dola, na kwa kuainisha namna na taratibu za utekelezaji wa mamlaka ya vyombo hivyo* na ndipo inapoanza na 'K' kubwa na kutanabaisha kuwa

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; hata hivyo pamoja na maana tajwa hapo juu, tunaungana na wanazuoni wengi waliowahi kusema Katiba;

- Ni waraka wa kisiasa unaowawezesha wananchi kujitambua kama taifa;
- Ni waraka wa kiutawala unaoeleza mgawanyo wa madaraka na majukumu ya vyombo mbalimbali vya Dola
- Ni waraka wa kisheria unaoongoza shughuli zote kisheria ambao ndio msingi wa sheria zote nchini au kwa lugha rahisi ;ni sheria Mama
- Ni muafaka wa kitaifa juu ya namna ya kuendesha mambo katika nchi

### 1.2 Maana ya Serikali za Mitaa:

Kwa mujibu wa ibara ya 151 (1), ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali za Mitaa maana yake ni vyombo vya kiserikali vilivyoundwa kwa majibu wa ibara ya 145 ya katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania kwa madhumuni ya kutekeleza madaraka ya umma.

Sheria ya Serikali za Mitaa Tanzania, iliundwa mwaka 1982 baada ya Sheria ya Madaraka Mikoani ya mwaka 1972 kuonekana kuwa ina ufanisi mdogo.

## 2. Hali Halisi ya Serikali za Mitaa

Pamoja na kwamba Serikali za Mitaa zinatambulika na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama inavyoeleza muundo na kazi za serikali hii katika ibara ya 145 na 146 ya katiba ya jamhuri ya muungano, bado muundo na utekelezaji wa serikali hii si huru kama zilivyo serikali nyingine hususan Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hivyo kupelekea kwa kiwango kikubwa kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Hii inadhihirishwa na malalamiko ya juu ya viwango vya chini vya huduma za jamii ngazi ya jamii na changamoto za ki utendaji na uongozi zinazoelezewa na viongozi na watendaji wa Halmashauri mbalimbali hususan utata wa kimuundo, kuingiliwa kimaamuzi, uwalakini kwenye mipango shirikishi na kutokuwa huru kwenye Mapato na Matumizi ya Rasilimali. Hata hivyo, pamoja na changamoto tajwa mara nyingi wengi wa viongozi wa Serikali za Mitaa wameshutumiwa kuwa hawawashirikishi wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao kutokana na ukweli kwamba hakuna vifungu vya kikatiba ambavyo vinawabana kufanya hivyo.

Ibara ya 6 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977, inafafanua kuwa serikali ni pamoja na serikali za mitaa na pia mtu anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote. Hivyo basi katika kutekeleza shughuli za serikali, Tanzania tuna ngazi mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Serikali za Mitaa. Kwa upande wa Zanzibar, kuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali za Mitaa.




Vile vile ibara ya 145 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazipa Serikali za Mitaa uhalali ya kwamba kutakuwa na vyombo vya Serikali za Mitaa katika kila mkoa, wilaya, mji na Kijiji na kwamba vyombo hivi vitakuwa vya aina na majina yaliyowekwa na sheria iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi.




## 3. Madai ya Awali ya Wananchi kuhusu Ufanisi wa Serikali za Mitaa

Baada ya kupewa fursa ya kisheria kupitia kazi ya Tume ya Mabadiliko ya katiba ya ukusanyaji wa maoni, Policy Forum iliunda Baraza la Katiba ambalo lilishirikisha wanachama na wananchi mbalimbali na kuweza kuwasilisha mapendekezo yake kwa Tume ambayo yalisheheni madai,matarajio na ushauri wa kila aina hususan jinsi gani ya kuboresha muundo na Ufanisi wa Serikali za Mitaa .Baadhi ya madai hayo yalikuwa kama ifuatavyo:-

## Madai Makuu

- Kuwe na muundo wa Serikali za Mitaa zilizogatuliwa
- Kuwa na serikali za mitaa zisizoingiliwa na serikali kuu bali ziwe na uhuru wa kuamua mambo yao wenyewe (fedha na wafanyakazi)
- Kuwa na serikali yenye ngazi mbili, Serikali za Mitaa na Serikali Kuu
- Kumtambua mwananchi kama msingi wa mamlaka yote




## Madai Mengineyo

- kutekeleza kazi za serikali za mitaa katika eneo lake
- kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi
- Kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kuitumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi

- Kuwapa wananchi madaraka zaidi ya kujitawala wenyewe, ushirikishaji na kudumisha demokrasia
- Kutambua haki za jamii ya kusimamia mambo yao wenyewe
- Kulinda haki za watu wachache
- Kuimarisha uwiano katika kutumia rasilimali
- Kuimarisha utoaji wa huduma za jamii katika ngazi ya chini
- Kuimarisha dhana ya kusimamia na mgawanyo wa madaraka
- Kuimarisha dhana ya usawa wa kijinsia katika ngazi za chini
- Kuweka utaratibu wa kuwawajibisha viongozi na watendaji wa serikali za mitaa

## 4. Masuala Mazuri yaliyomo Kwenye Rasimu ya Katiba ya 2014.

Pamoja na kwamba katika Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuna fasiri ya serikali za Mitaa na madaraka na uhuru wake haujawekwa wazi bali imewekwa misingi ya kuundwa kwake na hivyo uhuru na ufanisi wake umelekezwa na rasimu.

Mamlaka ya serikali za mitaa yamebainishwa katika sura ya sita ibara ya 68 (1) na (2) ya rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba *''serikali za nchi washirika, katika kutekeleza mamlaka zao, zitawajibika kustawisha mamlaka ya wananchi kwa kugatua madaraka kwa serikali za mitaa zitakazoanzishwa kwa mujibu wa katiba ya Tanganyika au katiba ya Zanzibar kama itakavyokuwa''.*



Rasimu pia imetambua umuhimu na ulazima wa wananchi kushiriki katika shughuli za serikali (Ibara ya 6 (d)). Pia, katika ibara ya 34 inatoa haki ya kila mwananchi kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi. Ibara hizi ni zinaruhusu au zinatoa fursa kwa serikali za washirika wa Muungano kuchukua hatua za makusudi kustawisha mamlaka za wananchi ngazi ya jamii kupitia serikali za mitaa.

Katika ibara ya 13 (1)(a)(ii),(iv) na ibara 13(2)(e) ya rasimu ya mabadiliko ya katiba imetambua umuhimu wa Viongozi na watumishi wa umma kuheshimu wananchi na ofisi walizokabidhiwa kuziongoza,vilevile umuhimu wa kutoa huduma kwa umma kwa kufuata misingi ya uadilifu na nidhamu.

Ibara ya 30(1)(b) inasema *''kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu;*

*-matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi;*
*-utekelezaji wa mamlaka ya nchi kuhusu sera za kitaifa na shughuli ya maendeleo ya jamii, na*

*-masuala mengine muhimu kwa jamii''*. Taarifa hizi haziwezi kumfikia mwananchi wa kawaida anayeishi ngazi ya msingi/jamii ki urahisi bila kuwepo muundo mzuri wa uongozi na utawala kutoka serikali ya Muungano na Serikali ya Nchi Mshirika hadi ngazi ya Mtaa, Kijiji na kitongoji.

Ibara ya 51(3) kila mtu anao wajibu wa kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na mali yoyote inayomilikiwa kwa pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu,na kuendesha

uchumi wa Taifa kwa makini kwa kuzingatia mipango endelevu na haki ya vizazi vijavyo. Ibara hii inaelezea wazi umuhimu wa kuwepo kwa Serikali za Mitaa ambazo maamuzi yake yanafanywa na kumilikiwa na wananchi. Hii itasaidia kuwepo kwa uzalendo na utaifa baina ya wana vijiji, mitaa na vitongoji hadi kupenda kutunza na kulinda mali za umma badala ya kudhaniwa ni mali ya serikali pekee.




Ibara ya 184(1) a; d; e na f imeainisha misingi mikuu ya utumishi wa umma mfano; uwajibikaji wa viongozi kwa makosa yanayofanyika chini yao, kuitikia matakwa na mahitaji ya watu kwa haraka na kwa wakati unaofaa, ambayo ni muhimu katika utendaji wa serikali za mataa.

Ibara ya 10(c)(iii) na (v) inahusu malengo makuu ambayo ni msingi mzuri kwa maendeleo ya wananchi kupitia serikali za mitaa kwasababu shughuli zilizoainishwa kwenye vifungu hivyo si za Serikali ya Muungano bali Serikali washirika kupitia Serikali za Mitaa. Hata hivyo ibara ya 11(1) inasisitiza kwamba malengo yote yaliyoainishwa na katiba ya jamhuri ya muungano yatakuwa mwongozo katika matumizi na kutafsiri masharti ya katiba ya Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na sheria nyingine yoyote na katika utekelezaji wa uamuzi wa kisera ili kujenga jamii iliyo bora na makini.




Ni matarajio yetu kuwa ibara na vifungu vilivyotajwa hapo juu vitazilazimu Serikali Washirika wa Muungano yaani Tanganyika na Zanzibar kugatua madaraka kwa serikali za mitaa ili kuziwezesha kuwa huru na kutumikia wananchi kwa misingi ya uadilifu, shirikishi na unyenyekevu wa hali ya juu.

Kama ilivyokuwa kwenye katiba ya mwaka 1977 kwenye ibara ya 8; sasa ibara hiyo imehamishwa kama ilivyo na kusomeka kama Ibara ya 6 ya rasimu ya katiba nayo juu ya mamlaka ya wananchi inasema; *"Jamhuri ya Muungano ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia haki ya kijamii, na kwa hiyo*

- *Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake kutoka kwa wananchi ambao kwa umoja na ujumla wao wanaimiliki na kuipatia katiba hii uhalali*
- *Lengo kuu la serikali litakuwa ni maendeleo na ustawi wa wananchi*
- *Serikali itawajibika kwa wananchi: na*
- *Wananchi watashiriki katika shughuli za serikali kwa mujibu wa masharti ya katiba hii".* Ni faraja kwamba ibara hii ndio jibu la wazi kwa madai ya wananchi kuhusu kutambuliwa kwao kuwa ndio msingi wa mamlaka (angalia dai namba nne kwenye madai makuu hapo juu)

## 5. Upungufu kwenye Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Pamoja na misingi na mambo mazuri yaliyowekwa kwenye rasimu ya Katiba ni vema kutanabaisha kuwa bado kuna upungufu ambao Bunge Maalumu la Katiba linapaswa kujadili na kufikia muafaka wa kuboresha kwa kuzingatia hoja za wananchi na misingi iliyowekwa ndani ya rasimu.Hapa tunaorodhesha masuala machache:-

- Madhumuni ya kuwepo kwa Serikali za Mitaa hayajaainishwa kwenye rasimu

- Ibara ya 68 (2) ya rasimu ya Katiba haizilazimishi serikali zote mbili za washirika wa Muungano kuwa na Serikali za Mitaa kwani kuna matumizi ya neno 'au' badala ya 'na'
- Serikali za Mitaa hazijatambuliwa vema katika rasimu kwani pamoja na mwongozo kuwa zitaundwa na Serikali za nchi Washirika, ibara ya 254 imefafanua maana ya serikali kuwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuacha kutoa ufafanuzi wa maana ya Serikali za Mitaa

## Mapendekezo

- Katiba itamke wazi kwamba kuwe na ngazi mbili katika nchi wa shirika (Serikali kuu na Serikali za Mitaa) zenye uhuru wa mamlaka na maamuzi.
- Kuwepo na kifungu kinachoeleza madhumuni ya kuwepo kwa serikali za mitaa: kuwa ni kupeleka madaraka kwa wananchi, kutambua uwepo wa serikali za mitaa kimuundo na kimajukumu.
- Katiba iweke kifungu kitakachoweka utaratibu utakao walazimisha viongozi wa serikali kuu kuheshimu maamuzi ya vikao halali vya serikali za mitaa vilivyoainisha vipaumbele vya wananchi, na hivyo ndivyo vitengewe rasilimali na si kuwabadilishia
- Kuwekwe kifungu kinachotamka serikali za mitaa zisiingiliwe na serikali kuu na ziwe na uhuru kamili wa kujiamulia mapato na matumizi ikiwemo wajibu wa kuchangia hazina ya serikali kuu ya nchi washirika

## Hitimisho

Kitendo cha kuwekwa kwa ibara kadhaa ndani ya rasimu ya katiba ya Jamhuri ya Muungano zenye kuashiria mamlaka ya wananchi na ulazima wa kugatua madaraka kwa serikali za mitaa ni ishara nzuri na ni jambo la lazima kwa Bunge maalumu la Katiba kuhakikisha ibara hizi zinalindwa na kubaki kuwa sehemu ya Katiba itakayopendekezwa.

Hata hivyo bado tunaona upungufu na dalili za kuendelea kwa changamoto zilizopo hivi sasa endapo Katiba mpya haitatoa mwongozo kamili wa kushughulikiwa kwa kero na changamoto hizo.

Hivyo basi, ufanisi wa Serikali za Mitaa utategemea na muundo utakaopendekezwa na Bunge Maalum la katiba kama ni serikali tatu lazima katiba ya Tanganyika na ya Zanzibar ifafanue malengo, madhumuni ya serikali za mitaa zilizopo ila iwapo itakuwa serikali mbili au moja utatakiwa mda wa kutengeneza serikali za mitaa.

## REJEA –

JMT (1977) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, dar es salaam

JMT (2013) Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dar es salaam

JMT (2014) Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dar es salaam

Policy Forum (2012) Katiba Mpya na Ufanisi wa Serikali za Mitaa Tanzania

JMT (1982) Sheria ya serikali za Mitaa, Dar es salaam

Policy Forum (2011) Mwongozo wa Katiba kwa Raia, toleo la 2012, Dar es salaam

JMT (2012) Sheria namba 8 ya Mabadiliko ya Katiba sura ya 83

policy forum

Plot 14, Sembeti Road
Off Old Bagamoyo Road,
Mikocheni B, P.O. Box 38486
Tel: +255 22 2780200
Mobile: +255 782 317 434
www.policyforum.or.tz
email: info@policyforum.or.tz